**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/EZ/2024/14**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000271**

**KATI YA**

**SSR POLYPLAST PRIVATE LIMITED ............................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) .......................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA leo tarehe 5 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 5 mwezi Februari 2025 kwa madai kwamba Mlalamikiwa aamriwe kutositisha huduma ya umeme kutokana na ankara ya kiasi cha TZS 6,625,002.60.

Mlalamikaji anaeleza kwamba alipokea ankara ya umeme tarehe 7 Novemba 2024 ya kiasi cha TZS 6,625,002.60 ambayo ni sawa na kV370 ingawa matumizi ya umeme katika kiwanda chao ni kV 10 kwa mwezi mmoja kwa sababu matumizi yao ni madogo. Mlalamikaji anaendelea kueleza kwamba baada ya kupokea ankara bishaniwa, alienda ofisi ya Mlalamikiwa kwa lengo la kupata muafaka wa ankara hiyo.

Mlalamikaji anaeleza kwamba kiwanda kilisitisha kufanya kazi hivyo kwa mwezi ambao wamepokea ankara ya Mlalamikiwa kiwanda hakikufanya shughuli za uzalishaji hivyo aliiomba ofisi ya Mlalamikiwa kupunguza ankara hiyo na ampatie ankara sahihi lakini hawakuweza kufikia muafaka na Mlalamikaji aliamua kuwasilisha malalamiko yake katika Mamlaka (EWURA) kwa ajili ya utatuzi.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, mnamo tarehe 18 Novemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (*EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020)*) GN. 428/2020.

Mnamo tarehe 6 Desemba 2024, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji na kueleza kwamba Mlalamikaji anapaswa kulipa ankara yake kwa maana imetokana na matumizi yake kwa mwezi Oktoba 2024. Mlalamikiwa ameendelea kueleza kwamba Mlalamikaji anapaswa kuthibitisha madai yake.

Kikao cha usuluhishi kilifanyika mnamo tarehe 7 Januari 2025 katika ofisi ya EWURA Kanda ya Mashariki Jengo la PSSSF Ghorofa ya Nne, Dar es Salaam. Katika kikao hicho, Mlalamikaji alieleza kwamba alitembelea ofisi ya Mlalamikiwa na kukutana na Mhasibu na kufanya nae mazungumzo na mwishoni alieleweshwa juu ya matumizi yake, hivyo aliamua kulipa ankara bishaniwa yote ili kuendeleza uhusiano mzuri na ofisi ya Mlalamikiwa. Hivyo basi Mlalamikaji aliandika barua na kuitaarifu Mamlaka kuwa ameondoa malalamiko yake.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yaondolewe na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 5 mwezi Februari 2025.

..........................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**